**NAMBA 5: MARKO 6:45-56. KUTEMBEA JUU YA MAJI – TOKA NJE YA MASHUA YAKO!**

Hiki ni kifungu ambacho kinatuambia kuhusu moja kati ya miujiza maarufu, ambayo Yesu aliifanya katika huduma yake. Ni kifungu ambacho kinatuambia kuhusu dhoruba nyingine kwenye bahari ya Galilaya, na kinatuonyesha uweza na nguvu ya Mungu katika maisha ya Yesu, wakati alipowatokea wafuasi wake kwenye ziwa. Kulikuwa na ripoti moja katika gazeti la Uingereza miaka michache iliyopita – na kichwa cha habari kilisema hivi: *"Yesu huenda kwa kweli alitembea juu ya barafu, si juu ya maji"!* Inavyoonekana, wanasayansi walikuwa wakitafiti hali ya mazingira karibu na bahari ya Galilaya, na wanaamini kuwa huenda wamepata maelezo juu ya muujiza huu. Wangeweza kusema kwamba kati ya miaka ya **mia tano** kabla ya Kristo na **mia tano** baada ya Kristo, kulikuwa na kipindi cha hali ya ubaridi katika Israeli, ambapo barafu inayoelea inaweza kuwa ilikuwa imejieneza na kutanda juu ya ziwa. Kwa hiyo, Yesu hakutembea juu ya maji, bali alitembea juu ya barafu tu! Watu wengi duniani leo wana uharaka wa kujaribu kuieleza jinsi miujiza ilivyotokea. Kwa kweli, kwa zaidi ya karne, wana-sayansi wetu wamekuwa wakijaribu kuieleza jinsi miujiza mingi ya kibiblia ilivyotokea.

Baadhi ya watu wangeweza kusema kuwa Mungu hakutenganisha maji ya Bahari ya Shamu, ili Waisraeli waweze kutembea katikati yake. Badala yake, walitembea katika eneo la bahari ambalo lilikuwa halina kina sana. Watu wengi watasema kwamba ufufuo wa Yesu haukuwa ni muujiza. Badala yake wanajaribu kusema kwamba kwa kweli Yesu hakufa msalabani; bali alipoteza fahamu tu, lakini baadaye, alipokuwa kaburini, alipata tena fahamu, na kisha alikuwa na uwezo wa kulisukuma nyuma jiwe, kisha akapigana na walinzi wa Kirumi, na baadaye akakimbia kwenda kwa Waisraeli, ili kuwashawishi watu kuwa alikuwa amefariki na kisha akafufuka! Kwa kweli, watu wamekuwa wakijaribu kuielezea jinsi miujiza katika Bibilia ilivyotendeka kwa sababu hawaamini yale yaliyotokea.

Lakini muujiza ni kitu ambacho kiko kinyume na sheria za asili; muujiza ni kitu ambacho si cha kawaida – si cha ulimwengu huu. Katika nchi za Magharibi, watu wengi hawaamini katika miujiza. Watu wengi hawamwamini Mungu. Na hivyo, wanaposoma kuhusu miujiza katika Biblia, hawai-amini. Sisi kama Wakristo, tunaombwa kuiamini miujiza. Na tunajua kwamba Mungu anaweza kufanya mambo yasiyo ya kawaida; anaweza kufanya mambo ambayo yanaonekana kuwa magumu kwetu. Na hapa katika sura hii tunaona kwamba kuna miujiza mingi: Yesu alikuwa amelisha kimiujiza watu **elfu tano**. Kisha Yesu anatembea juu ya maji.

Katika injili ya **Mathayo**, pia tunaambiwa kuwa Petro anatembea juu ya maji kwa muda mfupi. Na kisha, katika **mstari wa hamsini na moja**, tunaona kwamba wakati Yesu alipoingia kwenye mashua, upepo ulitulia na kila kitu kwenye ziwa kilikuwa shwari. Na kisha katika **mstari wa hamsini na sita** tunaona kwamba "*wote waliomgusa Yesu waliponywa".* Yesu anaweza kuponya magonjwa na kutoa pepo; Yeye anaweza kuwafanya viwete watembee na vipofu waone. Kwa hiyo, tunaweza kujifunza nini kutokana na kifungu hiki, na ni mambo tunaweza kuyahusisha kwetu leo?

Ulishaji wa watu **elfu tano** ulikuwa umeisha tu - na umati ulikuwa unaanza kutawanyika. Wanafunzi walikuwa wamemaliza kukusanya mabaki ya vyakula. Na Yesu, ambaye alikuwa amechoka baada ya huduma ya siku nzima, alitaka kutumia muda kadhaa wa kukaa peke yake, na Baba yake - na hivyo anaenda kwenye milima kuomba. **Katika mstari wa arobaini na sita**: "*baada ya kuwaacha alienda mlimani ili kuomba*". Na tunajua wazi kwamba hiki kilikuwa ni kitu, ambacho Yesu alikuwa akikifanya mara nyingi, na kitu alichohitaji kukifanya. Alihitaji kutumia

muda huo kuwasiliana na Baba yake. Kisha **Mstari wa arobaini na saba** unasema kwamba kwa wakati jioni ulipofika, mashua ilikuwa katikati ya ziwa, na yeye alikuwa peke yake katika nchi kavu. Tunajua kwamba Yesu alikuwa ameshawaambia wanafunzi wake kuingia kwenye mashua, na kuvuka ng'ambo ya ziwa. Lakini ilipokuwa jioni, wanafunzi walijikuta wakiwa katikati ya ziwa, wakipambana dhidi ya upepo na mawimbi. Upepo ulikuwa na nguvu sana kiasi, kwamba hawakuwa na uwezo wa kupiga makasia na kuvuka ziwa.

Pamoja na jitihada zao bora, walikuwa hawawezi kusogea karibu na mahali walipokuwa wakienda - tunaambiwa kuwa upepo ulikuwa kinyume nao. Labda unaweza pia kufikiria Petro akichukua hatua ya kushughulika hali hiyo! Anasimama mbele ya mashua na kupiga kelele kwa kutoa amri, na kuwaambia wanafunzi wapige makasia kwa bidii! Kwa vile Upepo ulivyo na nguvu; hawawezi kusikilizana. Kuna maji katika mashua, na wote wameloana kwa maji, kwa sababu ya mawimbi ambayo yanaingia kupitia upande wa pembeni mwa mashua. Watu wote wamechoka sana - na hawana furaha kabisa! Lakini kumbuka kwamba ingawa hali ni mbaya, wao walikuwa katika nafasi hii kwa sababu walikuwa watiifu kwa amri ya Yesu. Maana alikuwa amewaambia wavuke ziwa. Ulikuwa ni utii ambao ulikuwa umewaweka katika hali hiyo ngumu. Wakati Yesu alipowaambia wavuke ziwa, alijua kabisa kile kinachokwenda kutendeka. Alijua kwamba wangekumbana na hali hii ngumu. Na hivyo hawa hapa ni wanafunzi, wako mahali sahihi na kwa wakati muafaka. Wanatii amri yake. Wanayafanya mapenzi ya Mungu. Na bado wana wakati mgumu sana! Unajua nini, katika Afrika leo, kuna walimu wengi wa uongo wanaofundisha injili ya uongo katika makanisa yao. Hii inaitwa '*injili ya mafanikio*'. Na mafundisho haya yanasema kwamba maisha ya Kikristo ni maisha rahisi. Mafundisho yanasema kwamba kama wewe ni Mkristo, unapaswa kutarajia kuwa na afya na utajiri, na kwamba hakuna kitu kibaya kutokea kwako. Wanasema kama ukipata matatizo na majaribu, basi hiyo inamaanisha kuwa wewe uko nje ya uwepo wa Mungu. Hayo ndiyo wanayofundisha. Lakini mafundisho haya si ya kibibilia.

Angalia Ayubu, na Mtume Paulo, ili kuona kama mafundisho haya si ya kweli. Walipitia katika nyakati ngumu sana. Wote wawili walikaribia kufa kwa sababu ya ugonjwa. **Ayubu** alipoteza watoto wake, na mali zake, na wanyama wake wote. Je, alikuwa ametenda chochote kibaya? La hasha! Alikuwa akiishi maisha yake vizuri tu. Tabia yake ilimpendeza Mungu – lakini bado alikumbatana na mateso. **Paulo** aliteseka kwa ajili ya imani yake. Aliseswa kwa kuhubiri injili. Alipigwa. Alikamatwa na kuwekwa ndani. Kwa nini? Kwa sababu tu alikuwa anafanya kazi ya Bwana. Alikuwa anafanya kile ambacho Mungu alimtaka yeye akifanye. Kama utayatoa maisha yako kwa Kristo katika utii, daima kuna uwezekane wa tishio la kupata mateso. Labda, ni njia unayo-wajali wengine; kujitoa kwako katika kuishi kama Mkristo. Labda, kwa vile unavyojaribu kuwatumikia watu katika kanisa lako, utapata huzuni na maumivu. Kama Mchungaji mtiifu unaweza kukumbana na mateso;  aina ya mateso ambayo mtu ambaye si Mkristo, hawezi kukutana nayo. Magumu haya yote **hayamaanishi** kwamba tuko mahali pa makosa au pabaya. Haimaanishi kwamba tuko nje ya mapenzi ya Mungu katika maisha yetu. Wakati mwingine tunateseka kwa sababu tunayafanya mapenzi ya Mungu.

Kuwa watiifu kwa Mungu kunaweza kuleta dhoruba katika maisha yetu, kama ilivyofanyika kwa wanafunzi katika **Ziwa Galilaya –** lakini dhoruba hizi, na nyakati za mateso, zinaweza pia kuleta hisia za furaha katika maisha yetu. Hebu sikiliza nukuru hii kutoka mchungaji **Hughes** wa Amerika. *"Kama hautapanda mlima kamwe, huwezi kuumiza mguu wako - lakini wewe kamwe hautapata uzoefu wa furaha ya kusimama juu ya mlima".* Kama utachagua kutomtii Kristo, na badala yake, ukachagua njia rahisi katika maisha, unaweza kuzikosa baadhi ya dhoruba na mateso - **lakini** kamwe hautaujua uwezo wa Roho Mtakatifu katika maisha yako, katika

kukusaidia kukabiliana na matatizo yako. Kamwe hautaujua uwezo wa Roho Mtakatifu ukivuma ndani yako, ili kukufanya uwe imara katika dhoruba. Na kisha kuna mstari, ambao unatuonyesha kwamba, Yesu alijua kile kilichokuwa kinakwenda kutendeka pamoja na wanafunzi. **Marko sura ya sita, mstari wa arobaini na nane**: "*Yesu aliona wanafunzi wakihangaika kupiga makasia*". Yesu anaifahamu hali yao. Anaweza kuona kile wanachokipitia. Lakini angalia hata hivyo, kwamba yeye haionekani kuchukua hatua pale pale. **Mstari wa arobaini na nane** unatuambia kwamba "*ilipopata kama zamu ya nne ya usiku akawaendea, akitembea juu ya bahari – au ziwa*". Hiyo inamaanisha nini; "*zamu ya nne ya usiku"*? Warumi waliugawa usiku katika sehemu nne tofauti, na hii ilikuwa ni muhimu, hasa kama wewe ni askari katika jeshi. Wakati mwanajeshi alipokuwa kwenye zamu, akiillinda kambi wakati wa usiku, angeambiwa kuwa mlinzi wa usiku **kwa sehemu** ya usiku.

Sehemu ya kwanza ilikuwa kutoka **saa kumi na mbili** jioni hadi **saa tatu** usiku. Zamu ya pili ilikuwa **saa tatu** usiku hadi **saa sita** usiku. Zamu ya tatu ilikuwa **saa sita** usiku hadi **saa tisa** usiku, na zamu ya nne ya usiku ilikuwa **saa tisa** usiku hadi **saa kumi na mbili** alfajiri. Hivyo askari kufanya kazi kwa **masaa tatu** wakati wa usiku - kuangalia na kuwa makini na matatizo. Hivyo – Yesu anawaendea wanafunzi wake wakitembea juu ya maji, wakati wa zamu ya nne ya usiku; yaani saa tisa usiku hadi saa kumi na mbili alfajiri. Je, ni wakati gani Yesu aliwaambia wanafunzi kuingia kwenye mashua, na kuvuka ng'ambo nyingine ya ziwa? Je, **mstari wa arobaini na tano** anatuambia nini? "*Mara Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuingia kwenye mashua, na watangulie mbele yake kwenda Bethsaida".* Lakini hiyo haituambii ni wakati gani. Kwa hiyo, ni kitu gani kilitangulia kabla ya kifungu hiki? Kulisha ya watu **elfu tano**. Angalia **mstari wa thelathini na tano**: "*kwa wakati huu mchana ulikuwa umekwishapita, hivyo wanafunzi wakamwendea na kusema: tayari kumeshakuchwa, waamuru watu waende mbali, ili waweze kwenda na kujinunulia chakula".* Hiyo inamaanisha ulikuwa ni wakati wa kuchwa kwa mchana wakati, ambao muujiza huu ulitokea. Labda ilikuwa karibu **saa kumi** jioni.

Mara baada ya muujiza huu, Yesu anawaambia kuingia katika mashua - hivyo kwa wakati huu pengine ilikuwa **saa kumi na mbili** jioni – wakati wa **zamu ya kwanza ya usiku** wakati walopoanza safari yao katika mashua. Yesu sasa anakuja kwao wakati wa sehemu ya nne usiku – saa tisa hadi **saa kumi na mbili** alfajiri. Hiyo ina maana kuwa wamekuwa nje katika mashua, wakipambana dhidi ya mvua, na upepo, na mawimbi kwa karibu masaa **kumi na mbili** hivi! Lakini, mistari ya arobaini na saba na arobaini na nane inatuambia kwamba, wakati wa jioni ulipowadia, Yesu alikuwa mlimani, na alikuwa akiona jinsi walivyokuwa wakipambana na makasia. Unaona nini kuhusiana na hilo? Yesu anawaona akihangaika kwenye ziwa – lakini kwa karibu masaa **kumi na mbili** yeye hakuja kuwasaidia!! Ingawa anajua kuwa wanapambana na dhoruba, na licha ya kuwa anajua kuwa wanapita katika nyakati ngumu, anaamua kukaa mlimani ili kuomba!

Je, umewahi kujihisi kuwa wewe u peke yako, unaposhughulika na tatizo katika maisha? Labda umekuwa unahangaika na jambo fulani katika maisha au huduma yako. Labda kulikuwa na kifo katika familia. Huenda ukiwa kama mchungaji umekuwa ukikabiliana na jambo gumu katika Kanisa - nawe umeomba na kuomba juu yake, lakini hakuna chochote kilichotokea. Ilikuwa inaonekana kana kwamba sala zako zilikuwa zikipiga paa! Ilikuwa kana kwamba Mungu hakujua au hakuijali hali yako. **Na wewe ulijihisi hali ya kukata tamaa**. Huenda uko katika nafasi hiyo sasa. Unahitaji kujua kwamba Mwenyezi Mungu amesikia maombi yako. Yeye anajua kabisa mahali ulipo. Anazijua hofu na magumu yako. Yeye anakuona wewe unavyopambana na makasia. Lakini kwa sababu mbalimbali, tusizo-zijua sisi, inaturuhusu kupita kwenye mabonde haya ya ugumu, sio kwa sababu hajali - lakini kwa sababu ana lengo

nasi ambalo hatuwezi kuliona. Yeye anakuona wewe unavyopambana, na atakuja kukusaidia, lakini hatakuja mara moja. Atakuja kwa wakati wake. Ana lengo.

Angalia katika **mstari wa arobaini na tisa**: ni lazima ilikuwa ni kitu cha kutisha sana, kwa wanafunzi kuona kivuli cha mtu akitembea juu ya maji, katika giza. **Mstari wa hamsini** unatuambia kuwa walikuwa wamejawa na hofu! Hata wakapiga kelele; walipiga kelele kwa sababu walidhani ulikuwa ni mzimu. Waliogopa. Lakini, angalia jibu la Yesu katika **mstari wa hamsini**: *"Iweni wajasiri! Ni mimi. Msiogope".* Katika injili ya **Mathayo**, anatumia jina la Mungu la Agano la Kale. "*Mimi niko*". Yesu anasema, Usiogope, ni mimi niko pamoja nanyi. Huu si mzimu ukitembea juu ya maji – huyu ni Mwana wa Mungu mwenyewe. Hakuna haja ya kuwa na hofu, kwa sababu Mungu yupo hapa. Je, Mungu wako ni mkubwa kiasi gani? Je, yeye ni mkubwa wa kutosha kukulinda wewe?

Shida tuliyo nayo katika maisha ni kwamba, mara nyingi huwa tunaogopa, na tunahoji kama Mungu anaweza kutulinda sisi. Wakati mwingine tunaishi katika hofu, kwa sababu tunadhani kila kitu kinatutegemea sisi. Hatuna uhakika kama tunaweza kumwamini Mungu kutusaidia katika maisha yetu. Mungu wetu ni Mungu wa ajabu ambaye aliumba ulimwengu wote - na kama yu pamoja nasi, hatuhitaji kuwa na hofu. Katika nguvu zake tunaweza kukumbana, na majaribu, na mapambano ambayo yanaweza kuja upande wetu - lakini tunahitaji kujifunza kumwamini na kumtegemea yeye ili atusaidie. Kabla ya kuhitimisha, ninaomba turejee katika injili ya Mathayo - kwa sababu anataja kitu ambacho Marko haja-kitaja. Turejee katika **Mathayo sura ya kumi na nne** na tusome mstari wa **ishirini na nane hadi thelathini na mbili**. Tuna hadithi hii ya kushangaza ya imani, iliyoandikwa na Mathayo kuhusu mtu mwingine, ambaye anatembea juu ya maji!  Tunasoma kuhusu Petro akifanya jambo la kimiujiza.

Hiki ndicho anachomwambia Yesu: *"Bwana, kama wewe ni kweli, Petro alijibu, niambie ili nije kwako juu ya maji. Njoo, Yesu alisema. Na Petro akashuka kutoka kwenye mashua, akitembea juu ya maji, na kuja kwa Yesu".* Kweli?! Hilo ni jambo la kishujaa la kufanya, sivyo? Fikiri juu ya hilo. Hii ilikuwa ni dhoruba ya hatari. Mawimbi yalikuwa makubwa. Upepo ulikuwa na nguvu. Na ilikuwa bado ni giza. Labda ulikuwa mwanzo wa kupata mwanga. Unaweza kufikiria kama ungekuwa niwe ukiwa katika Ziwa Victoria wakati wa usiku katika dhoruba - na kivuli kinakuijia kukuelekea wewe juu ya maji - na ukasikia sauti ikikuambia, "*njooni kwangu*". Ungefanya nini? Nadhani itakuwa vigumu sana kufanya - hata kama ingekuwa ni wakati wa mchana, ambapo ziwa likiwa limetulia. Nafikiri tunapaswa kumpa sifa Petro hapa. Mara nyingi tunamkosoa yeye kwa sababu ya makosa yake – lakini hapa katika Ziwa Galilaya katikati ya dhoruba, anamtii Yesu na anadiriki kutoka nje ya mashua, ndani ya maji. Hii ni hatua kubwa sana ya imani.

Petro yuko ukingoni mwa mashua, na upepo unavuma kwa nguvu. Utachagua nini? Kutoka nje ya mashua na kushuka ndani ya maji - au kukaa katika mashua? Nadhani wengi wetu tungeweza kuchagua kukaa katika mashua, mahali ambapo palikuwa salama kidogo. Lakini Petro, baada ya kualikwa na Yesu na kuchukua hatua ya kutoka nje ya mashua, na kutembea juu ya maji, anachukua hatua ya ajabu ya utiifu, na imani. Na kwa muda mfupi, Petro anakuwa mtu wa pekee, ukimwondoa Yesu, kutembea juu ya maji ! Je, unaweza kufikiria jinsi alivyojisikia? Alipata uzoefu wa nguvu za Mungu, katika maisha yake alipokuwa akitembea juu ya maji – lakini alipata uzoefu wa nguvu za kimiujiza, kwa sababu alichukua hatua ya hatari kwa kutoka kwenye mashua.

Na wewe je? Vipi kuhusu mashua yako? Wakati mwingine tunahisi kwamba ni salama kwetu kubaki katika mashua yetu ndogo, na hatutaki kutoka nje. Tunafarijika kuwa pale tulipoi, na

tunataka kukaa mahali ambapo penye faraja na usalama. Je, ni vipi kama Mungu ataongea na wewe katika maisha yako, na kukutaka kufanya kitu ambacho kinakutia hofu? Je, utakataa mwaliko wake? Au utachukua hatua hiyo ya imani, na kutoka nje ya maisha yako ya starehe – na kuchukua hatua ya hatari ya kuloana kwa maji katika ziwa? Labda, Mungu amekuwa akikutia changamoto kuhusiana na hili katika huduma yako. Labda, umehisi Mungu akiongea katika maisha yako, akikuomba ufanye kitu tofauti kwa ajili yake. Labda amekuwa akikuomba uwe mtiifu kwake, katika sehemu fulani ya maisha yako na katika huduma – lakini bado hujataka kutii, kwa sababu inaonekana kukutisha. Ni hatari. Utafanya nini? Kukaa katika mashua yako - au kuchukua hatua hiyo ya utii na kutoka nje ya mashua yako? Ndiyo, itakuwa inatisha kutoka nje ya mashua yako, na unaweza hata kuwa na hofu wakati mwingine, lakini tunapaswa kukumbuka kwamba tunaye Mungu pamoja nasi wakati wote. Je, Yesu aliwaambia nini wanafunzi? "*Iweni na ujasiri! Niko hapa. Msiogope".* Ndiyo, unaweza hata kushindwa mara chache, kama vile Petro alivyofanya - lakini je, Mungu atajitenga na wewe kwa sababu ya hiyo? Hapana! Bila shaka hapana. Je, Yesu alimwacha Petro wakati alipoanza kuzama majini? **Mstari wa thelathini na moja** unasema nini? "*Mara moja, Yesu aliu-onyosha mkono wake na kumshika*". Alimwokoa asizame, hata kama alifanya makosa.

Kwa nini Petro alianza kuzama? Angalia katika **mstari wa thelathini**: *"alipouona upepo, aliingiwa na hofu, pale alipoanza kuzama, alipiga yowe, Bwana niokoe".* Ilikuwa ni hofu ambayo ilimsababisha Petro kuogopa. Wakati alipotazama karibu naye, alimtazama Yesu kwa mbali, na aliingiwa na hofu. Na mara nyingi sana ndivyo ilivyo hata kwetu. Tunapoangalia mbali na Yesu, tunaangalia woga wetu badala ya kumwamini Mungu. Kuna wimbo ambao wakati mwingine tunaimba katika makanisa yetu. *"Elekeza macho yako kwa Yesu; mwangalie kamilifu katika uso wake wa ajabu, na mambo ya dunia yatakua yanafifia kwa ajabu, katika nuru ya utukufu na neema yake".* Tunahitaji kuyaelekeza macho yetu na kumwangalia Yesu. Leo, miaka elfu mbili baada ya Yesu kumwalika Petro atembee juu ya maji, yeye anatualika mimi na wewe kufanya hivyo. Yeye hatulazimishi sisi. Yeye anatuita, na anatualika sisi kushiriki katika kumfuata Yeye, popote yeye popote anapoenda. Lakini hiyo inamaanisha kuchukua hatua ya hatari, na itahusisha imani.

Kila mara unapoondoka katika mashua yako, katika kumtii yeye, unakuwa imara katika imani yako - ili wakati mwingine anapokualika kufanya kitu kwa ajili yake, utamtii bila kuhojihoji. Je, utafanya nini? Katika maisha ya Kikristo tutaka-biliwa na matatizo, lakini Mungu anajua kuhusu mapambano yenu. Anaujua udhaifu wako. Anakujua wewe vyema - na yeye atakutia nguvu. Usiogope - kwa sababu yeye yu pamoja nawe. Na tuwe watiifu kwake. Hebu tutoke nje kwa imani, ili tumfuate Yeye mahali ambapo yeye anatuita kwenda.

Lakini, kumbuka hii, kama unataka kutembea juu ya maji, na kufurahia maisha na Yesu, unapaswa kutoka nje ya mashua yako. Kama wewe ukikaa katika mashua yako, huwezi kupata uzoefu na msisimko wa kutembea katika imani pamoja na Yesu. Je, kuwaomba ufanye nini leo? Kuna watu wengi katika makanisa yetu, ambao hawataki kuchukua hatua ya hatari, ya kulowanisha miguu yao kwa maji! Kuna wachungaji wengi ambao hawataki kulowanisha miguu yao! Lakini, hebu tulenge kumfuata Kristo, popote anakotaka kutuongoza, tukijua kwamba atatunza sisi njiani.